# KUJENGA NA KUIMARISHA UHUSIANO NA WADAU WA DLDM

5

## Utangulizi

Ushirikiano na wadau wa DLDM ni muhimu sana kwa maendeleo ya chama. Kujenga uhusiano kunaweza kuongeza uwezo wa chama kufikia dira na malengo yake. Ushirikiano na wadau pia unaweza kuongeza uelewa na ufanisi kwa njia ya kubadilishana ujuzi na uzoefu, kupata msaada wa nguvu kazi, vitendea kazi na hata fedha za kusaidia shughuli za chama.

Ili vyama vya watoa huduma wa DLDM vifanikiwe kuwawezesha wanachama wao kiuchumi, vinahitaji kujenga uhusiano mzuri na wadau mbalimbali katika sekta hii. Ili hili liweze kufikiwa, vyama vinahitaji:-

- Kuainisha wadau muhimu wa kushirikiana nao;
- Kuelewa uwezo wa wadau hao kitaasisi, mwelekeo wao, vipaumbele vyao vya maendeleo na taratibu zao hasa katika kutoa msaada;
- Kuainisha maeneo ya kushirikiana au kufanya kazi pamoja;
- Kuainisha shughuli maalumu au wajibu wa wadau hao.




*Umuhimu wa duka la dawa muhimu unaendelea kuonekana kama njia mbadala ya kufikisha huduma mbalimbali za afya kwa jamii.*

## Wadau muhimu wa DLDM

Wafuatao ni baadhi ya wadau muhimu ambao vyama vya watoa huduma wa DLDM vinaweza kushirikiana nao:

- Mamlaka zinazosimamia huduma za dawa hasa Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA) na Baraza la Wafamasia;
- Halmashauri ya wilaya hasa Idara ya Mipango, Idara ya Afya, Idara ya Biashara na Ushirika na mengineyo;
- Mfuko wa Bima ya Afya wa Taifa na Bima ya Afya ya Jamii;
- Programu za afya za taifa kama vile ya Uzazi wa Mpango, Malaria, UKIMWI, Kifua Kikuu, Ukoma nk;
- Vituo vya afya, zahanati na hospitali;
- Wadau wa maendeleo ikiwa ni pamoja na wafadhili na mashirika yasiyo ya kiserikali yanayofanya kazi katika sekta ya dawa;
- Wasambazaji na wauzaji wa jumla wa bidhaa za dawa na vifaa husika;
- Taasisi za mafunzo kama vile VETA;
- Taasisi za kifedha;
- Serikali za mitaa katika ngazi ya kata na kijiji;
- Vyombo vya habari.

## Maelezo juu ya wadau

### *(i) Mamlaka zinazosimamia sheria/kanuni*

Mamlaka muhimu zinazosimamia sheria ambazo zinafanya kazi kwa karibu sana na watoa huduma wa DLDM ni TFDA na Baraza la Wafamasia. Mamlaka zote mbili zimetokana na Bodi ya Famasia iliyokuwa na jukumu la kusimamia shughuli zote za sekta ya dawa. Wakati TFDA inashughulika na utoaji wa leseni na udhibiti wa ubora wa chakula, dawa, vipodozi na vifaa vya tiba, Baraza la Wafamasia lina jukumu la kusajili watendaji wa kifamasia na kudhibiti maadili ya kitaaluma.

*Wakati TFDA ina jukumu la kudhibiti ubora wa dawa na utoaji wa leseni, Baraza la Wafamasia lina wajibu wa kusajili wataalamu wa wa famasia na kudhibiti utendaji wa kitaalamu.*


Kuhusu mpango wa DLDM, Mamlaka ya Chakula na Dawa imekuwa na mchango mkubwa katika utekelezaji wa mpango huu. Mamlaka pia imekuwa mstari wa mbele katika kutangaza na kupandisha hadhi mpango wa DLDM na kusimamia upanuaji wake kitaifa. Hata hivyo, inategemewa kuwa Baraza la Wafamasia litakuwa na jukumu kubwa la kusimamia shughuli za mafunzo, maadili na ufanisi wa kitaalamu. Hivyo, baraza lina jukumu la kuratibu mchakato mzima wa kutengeneza mfumo wa elimu endelevu kwa watoa dawa wa DLDM, kuwatambua kama sehemu ya taaluma ya Famasia na kisha kusimamia shughuli za utoaji wa dawa.

*(ii) Halmashauri ya Wilaya*

Halmashauri ndiye msimamizi mkuu wa shughuli zote za maendeleo katika wilaya. Ni mahali ambapo maamuzi yote muhimu kuhusu wilaya yanafanyika kuhusu vipaumbele vya maendeleo na mahitaji ya utekelezaji, ikiwa ni pamoja na rasilimali watu, vifaa na fedha. Idara ya afya ya wilaya ni mdau mkubwa katika utekelezaji wa mpango wa DLDM. Idara nyingine ambazo vyama hivi vinahitaji kufanya nazo kazi kwa karibu ni Mipango, Biashara, Ushirika na Maendeleo ya Jamii. Mbali na kutoa msaada wa kiufundi, baadhi ya halmashauri tayari zimeanza kutenga fedha kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali za DLDM.

*(iii) Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya*

Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya ni mmoja wa wadau wakubwa katika utekelezaji wa mpango wa DLDM. Mfuko huu hushirikiana na DLDM kwa ajili ya kutoa huduma kwa wateja wake. Pia imesaidia kuhamasisha wanachama wake kuhusu huduma za DLDM. Hata hivyo, kumekuwa na changamoto hasa kuhusu ulipwaji wa gharama za huduma ambazo maduka yanatoa kwa wanachama wa mfuko huo, jambo ambalo limesababisha baadhi ya maduka ya dawa muhimu kusimamisha huduma hiyo. Hii ni sehemu mojawapo ambayo vyama vya watoa huduma wa DLDM vinaweza kujadiliana na mfuko huo ili kuhakikisha kuwa huduma hizo muhimu zinakuwa endelevu.




*Kutokana na matumizi ya DLDM yanayoongezeka kama njia ya kuifikishia jamii huduma za afya zinazosimamiwa na programu za afya za taifa, vyama vya watoa huduma wa DLDM vinaweza kutumia furasa hii kujenga uhusiano na wadau hao.*

### *(iv) Mfuko wa Afya wa Jamiii*

Ni mpango wa hiari unaoiwezesha kaya kulipia huduma za afya wakati wanapokuwa na fedha badala ya wakati wa ugonjwa. Hivyo, wanachama wa Mfuko wa Afya wa Jamii hawalipii matibabu ili wapate huduma katika zahanati, vituo vya afya na hata hospitali za wilaya. Ada zinazolipwa na wanachama huwa zinaamuliwa katika ngazi ya halmashauri, na jumla ya mapato yaliyokusanywa kutoka kwa wanachama yanaunganishwa na ruzuku kutoka serikali kuu kwa ajili ya kuimarisha huduma za afya vijijini. Uzoefu unaonesha kuwa baadhi ya halmashauri hutumia makusanyo kutoka katika huo mfuko kuboresha huduma hasa ya dawa. Vyama vya watoa huduma wa DLDM vinahitaji kutafuta uwezekano wa kufanya shughuli pamoja na mfuko huu ili kuongeza utumiaji wa DLDM kwa wanachama wa mfuko wa afya ya jamii.

### *(v) Programu za afya za taifa*

Maduka ya dawa muhimu yameendelea kuwa kivutio kwa programu nyingi za afya za taifa na yanatumika kama njia mojawapo ya kuifikishia jamii huduma mbalimbali za afya. Mwaka 2006 maduka ya dawa muhimu ya mikoa ya Morogoro na Ruvuma yalifanyiwa majaribio ya kusambaza dawa mseto ya malaria. Matokeo ya majaribio hayo yamesaidia kufikia uamuzi wa kutumia maduka ya dawa muhimu kusambaza dawa mseto kwa bei nafuu nchini chini ya usimamizi wa mpango wa kusambaza dawa mseto za malaria zenye bei za ruzuku (AMFm). Pia maduka hayo yanasambaza dawa aina ya Zinc na ORS kwa ajili ya kutibu magonjwa ya watoto ya kuharisha. Programu nyingine ambazo zimeonesha mafanikio ya kutumia maduka hayo ni Uzazi wa Mpango, UKIMWI, Kifua Kikuu na Ukoma. Kuongezeka kwa shauku ya programu nyingine za afya kutumia maduka hayo kunatoa fursa kwa vyama hivi kufanya kazi kwa karibu na programu hizo.

### *(vi) Vituo vya huduma za afya*

Uzoefu umeonesha kuwa wateja wengi hasa sehemu za vijijini, kabla ya kuhudhuria vituo vinavyotoa huduma za afya kama zahanati, vituo vya afya au hospitali, hupitia kwanza kwenye duka la dawa. Wakati huo wagonjwa wengi wanaonunua dawa za vyeti katika maduka hayo hupata vyeti hivyo kutoka katika vituo hivyo vya afya. Hii inadhihirisha umuhimu wa uhusiano uliopo kati ya maduka haya na vituo vya kutolea huduma za afya. Kwa hiyo, vyama vya watoa huduma wa DLDM vinahitaji kuainisha fursa mbalimbali za ushirikiano na vituo hivyo ili kuboresha huduma kwa wateja wao. Moja kati ya maeneo hayo ya ushirikiano ni huduma za rufaa kwa wateja hasa watoto wenye umri wa chini ya miaka mitano ambao huugua mara kwa mara.

> *Moja ya maeneo ambayo watoa huduma wa DLDM wanafanya kazi pamoja na vituo vya kutolea huduma za afya, ni rufaa ya wateja wa maduka hayo hasa watoto wenye umri chini ya miaka mitano ambao wako kwenye hatari zaidi kuugua.*

### *(vii) Wadau wa maendeleo*

Kundi hili linajumuisha mashirika ya kimataifa yasiyokuwa ya kiserikali ikiwa ni pamoja na wafadhili. Miongoni mwa mashirika hayo yasiyokuwa ya kiserikali na ambayo yamekuwa mstari wa mbele kusaidia mpango wa DLDM ni Shirika la Management Sciences for Health (MSH), Clinton Foundation, Population Services International (PSI-Tanzania), Family Health International (FHI), the Academy for Educational Development (AED) kupitia mradi wa POUZN, na Tanzania Marketing and Communications Company Ltd (T-Marc) pamoja na nyinginezo.

MSH ni mdau aliyefanya mengi kwa kufanya majaribio ya mpango wa DLDM katika Mkoa wa Ruvuma na kisha kuendeleza upanuzi wake katika Mkoa wa Morogoro, na kutoa msaada wa kiufundi kwa Mamlaka ya Chakula na Dawa katika azma ya kueneza mpango huu kitaifa. Shirika hili pia limekuwa mstari wa mbele kuhamasisha uanzishaji wa vyama vya watoa huduma wa DLDM. Pia limekuwa na mchango mkubwa sana katika kuandaa kitini maalumu kuhusu uanzishaji na uendeshaji bora wa vyama vya watoa huduma wa DLDM.

*Uhusiano wa karibu kati ya vyama vya watoa huduma wa DLDM na wauzaji wa jumla wa dawa, utasaidia kuongeza upatikanaji wa dawa bora na muhimu ambazo zinatumika sana na jamii inayohudumiwa na DLDM.*

Baadhi ya wafadhili waliochangia katika kufanikisha uanzishaji na upanuzi wa mpango huu wa DLDM ni: Mfuko wa Bill na Melinda Gates (Bill and Melinda Gates Foundation); Mfuko wa Dunia wa kupambana na UKIMWI, Kifua Kikuu na Malaria (GFATM); Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Watu wa Marekani (USAID); Shirika la Maendeleo la watu wa Denmark (DANIDA) na Rockefeller Foundation.

### *(viii) Wauzaji wa jumla wa dawa na vifaa mbadala*

Wadau hawa wana jukumu kubwa na la maana sana kuhakikisha upatikanaji wa dawa bora na vifaa vingine vinavyouzwa katika duka la dawa muhimu. Vyama vya watoa huduma wa DLDM vinahitaji kushirikiana kwa karibu sana na wadau hawa hasa katika upatikanaji wa dawa bora na muhimu ambazo zinatumika sana na jamii inayohudumiwa na DLDM. Kuwa karibu na wauzaji hao wa jumla kunaweza kusaidia vyama hivyo kufikia masharti nafuu zaidi ya biashara na wauzaji wa jumla, hasa wanachama wa DLDM wakiamua kufanya ununuzi wa pamoja.

### *(ix) Chuo cha Ufundi Stadi na Mafunzo (VETA)*

VETA ni taasisi inayojitegemea yenye jukumu kubwa la kuendeleza mafunzo ya ufundi stadi nchini. VETA inaendesha vyuo 11 vya mkoa na vituo vingine 10.

Wakati wa kufanya tathmini ya vyama vya watoa huduma wa DLDM Juni 2009, ilifahamika kuwa baadhi ya vyama hivyo hutumia kumbi za VETA kufanya mikutano yao. Lakini, hata hivyo, vyama hivyo vingefanikiwa zaidi kwa kufanya kazi kwa karibu sana na VETA kwa kuwaomba kutoa mafunzo ya

uendeshaji wa biashara hasa kwa wamiliki wa DLDM. Mafunzo kama hayo yanaweza kuwekwa katika vipindi vifupi vifupi na kutolewa ndani ya mwaka mzima. Sehemu ya ada itakayolipwa na wamiliki itachukuliwa na chama kwa kuendeleza mafunzo kama hayo, na hivyo kuongeza mapato ya chama, wakati huo huo ikijenga uwezo wa chama kifedha.

### *(x) Taasisi za fedha*

Taasisi za fedha zina jukumu kubwa katika kuendeleza mpango wa DLDM kwa kuwawezesha watoa huduma wa DLDM kuweka fedha zao na kuchukua mikopo. Taasisi hizo ni pamoja na benki za biashara, taasisi zinazotoa mikopo midogo midogo na SACCOs.

Mwaka 2008, Shirika la MSH liliingia mkataba na Shirika la Mennonite Development Associates (MEDA) kuunganisha wamiliki wa DLDM na taasisi za fedha katika maeneo yao na kuzishawishi taasisi hizo kutoa mikopo yenye masharti nafuu. Kutokana na shughuli hiyo, baadhi ya taasisi za fedha zililegeza masharti na kuwawezesha wamiliki wengi wa DLDM kupata mikopo ya kuendeleza biashara zao. Kwa hiyo, vyama vya watoa huduma wa DLDM vinahitaji kujenga uhusiano kama huo na taasisi hizo za fedha ili wanachama wao waweze kupata mikopo yenye masharti nafuu na hivyo kuongeza upatikanaji wa mitaji kwa ajili ya kuendeleza biashara ya DLDM.

*Vyama vya watoa huduma a DLDM vinahitaji kujenga uhusiano wa karibu zaidi na taasisi za fedha, ili kujenga mazingira yatakayowezesha kupata mikopo kwa masharti nafuu.*

### *(xi) Serikali ya kijiji na uongozi wa kata*

Viongozi wa serikali za mitaa katika ngazi ya kata na kijiji ni wawakilishi wa serikali kuu kwa jamii. Wana madaraka makubwa sana na wanaweza kutumika kuishawishi na kuihamasisha jamii. Wanao pia uwezo wa kusuluhisha migogoro katika jamii wakiwemo watoa huduma wa DLDM. Zaidi ya hayo wanasimamia shughuli zote za maendeleo katika ngazi hizi. Muundo huu pia una wajibu mkubwa katika mchakato wa kuandaa mpango wa maendeleo wa wilaya unaoanza katika ngazi ya kitongoji. Kwa hiyo, ni muhimu sana kwa vyama hivi kujenga uhusiano wa karibu na mamlaka hizi za utawala kwani maduka hayo ni sehemu ya jamii husika ndani ya mamlaka hizo.

### *(xii) Vyombo vya habari*

Jukumu la vyombo vya habari katika kutoa taarifa kwa jamii ni la muhimu sana. Baadhi ya vyombo vikuu vya habari ni radio, runinga, mtandao wa intaneti, magazeti ya aina mbalimbali na matangazo ya nje kama vile mabango. Tafiti nyingi zimeonesha kuwa radio ni moja ya vyombo vya habari ambavyo vinawafikia Watanzania wengi sana hasa sehemu za vijijini. Kwa hiyo, radio inafaa kutumiwa na vyama hivyo kwa kuwasiliana na wanachama au wadau wengine.

Sekta ya habari imekua kwa haraka kutokana na sera ya utandawazi ulioanza katika miaka ya 1990. Hali hii imechangia kuanzishwa kwa taasisi nyingi za habari za watu binafsi ikiwa ni pamoja na uchapishaji wa magazeti ya aina mbalimbali, stesheni za radio na televisheni zenye uwezo wa kufika sehemu mbalimbali. Pia wazo la radio za jamii sasa limeendelea kupanuka na hasa katika mashirika ya dini, na pia baadhi ya halmashauri zimeanzisha stesheni kama hizo.


*Radio ndiyo chombo cha habari kinachowafikia Watanzania wengi zaidi hasa sehemu za vijijini.*

Ikizingatiwa kuwa radio za jamii si za kibiashara, vyama vya watoa huduma wa DLDM vinahitaji kujenga uhusiano wa karibu sana na stesheni kama hizo, hasa zile ambazo zimeanzishwa na halmashauri na kuzitumia vizuri kuelimisha jamii juu ya DLDM na kuwafikia wanachama wao popote pale walipo. Hata hivyo, uhusiano huo usiishie kwenye radio za jamii tu bali upanuliwe zaidi na kuzihusisha stesheni nyingine kwa ajili ya kupanua mawasiliano na kuongeza matumizi ya DLDM.

## Maeneo ya ushirikiano na wadau

Kutokana na maelezo kuhusu wadau hapo juu, inaonesha wazi kuwa kuna taasisi na programu nyingi ambazo watoa huduma wa DLDM wanaweza kushirikiana nazo. Hivyo ni muhimu kuainisha maeneo ya kushirikiana ili kuviwezesha vyama kufaidika zaidi na ushirikiano huo. Maeneo kama hayo ni lazima yaainishwe kufuatana na malengo na madhumuni ya chama. Mchoro huu hapa chini unaonesha maeneo matano muhimu ya ushirikiano ambayo vyama vya watoa huduma wa DLM vinaweza kuzingatia katika kujiendeleza.

### *Maeneo ya ushirikiano*



## Majukumu ya wadau katika maeneo tofauti ya kushirikiana

Baada ya kuelezea wadau muhimu wa DLDM na maeneo ya ushirikiano, sehemu hii inaonesha jinsi wadau hao wanaweza kugawanywa kufuatana na maeneo hayo.

*Jedwali 1: Uwezeshwaji wa DLDM kupitia ushirikiano na taasisi mbalimbali*

| Kuwapa sauti | Kuendeleza uwezo wa kiufundi | Kuboreshaji utoaji wa huduma | Kuwezesha maendeleo ya kiuchumi | Uenezi na elimu kwa jamii |
|---|---|---|---|---|
| • Vyombo vya habari | • Mamlaka (TFDA, PC)<br>• Taasisi za mafunzo (k.m. VETA)<br>• Wadau wa maendeleo (mashirika ya ndani na nje)<br>• Halmashauri ya wilaya<br>• Programu za afya za taifa | • Mamlaka (TFDA, PC)<br>• Wauzaji wa jumla wa dawa<br>• Programu za afya za taifa<br>• Vituo vinavyotoa huduma za afya<br>• Mfuko wa Bima ya Afya wa Taifa<br>• Halmashauri ya wilaya hasa idara ya Afya | • Taasisi za fedha<br>• Wadau wa maendeleo<br>• Mfuko wa Bima ya Afya wa Taifa<br>• Halmashauri ya wilaya hasa idara za mipango, biashara na ushirika, na maendeleo ya jamii | • Vyombo vya habari<br>• Wadau wa maendeleo hasa mashirika yanayotumia njia za kisoko kufikisha huduma za afya kwa jamii (kama PSI, AED and T-Marc)<br>• Mamalaka (TFDA, PC)<br>• Wauzaji wa jumla wa dawa<br>• Mfuko wa afya ya jamii<br>• Halmashauri ya wilaya<br>• Programu za afya za taifa<br>• Serikali ya kijiji na uongozi wa kata |

*Imetolewa na Shirika la Management Sciences for Health (MSH) kwa ushirikiano na Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA).*
*Utayarishaji na usanifu wa kitini hiki umefanywa na Shirika la Medianet Ltd.*
*Shukrani za pekee ziwaendee Rockefeller Foundation kwa msaada wa kifedha.*